[R5436]

# WAKILI DHALIMU

***LUKA 16:1-13***

**"Aliye mwaminifu katika lililo dogo kabisa huwa mwaminifu katika lilio kubwa pia: na aliye dhalimu katika lililo dogo kabisa huwa dhalimu katika lililo kubwa pia" – (mstari).10.**

Kwa kuwa mafarisayo ndio walikuwa wakiongoza katika kuunga mkono sheria, yesu alilenga mifano yake mingi kinyume chao huku kwa kulinganisha , alipuuzilia mbali wayahudi wasio wa kidini – yaani masadukayo , ambao hawakukiri imani. Funzo la leo linaambatana na hii. Mfano hii ilitolewa kama kemeo kwa roho wa mafarisayo ambao waliwekea wengine mizigo mizito, lakini wao wenyewe wakaihepa huku wakijifanya watiifu sana wa sheria.

Katika nyakati za kale sana zaidi ya sasa, ilikuwa tabia ya watu matajiri kuchagua mawakili. Wakili kama huyo alikuwa na utawala yote ju ya mali ya bwana wake kama vile bwana mwenyewe; alikuwa na uwezo kama ya mkubwa. Baadhi ya hao mawakili walikuwa waminifu; wengine wabadhirifu. Yule aliyetajwa katika mfano wa bwana wetu alikuwa kwenye fujo tena adimu. Bwana wake alikuwa ameamua kuondoa huduma zake na akawa amemwambia apeane hesabu yake.

Kwenye vitabu vyake kulikuwa na wenye deni ambao walikuwa dhahiri kwamba waliachwa bila nafasi ya kuweza kufikiria wajibu wao. Huyo wakili alisema kwamba angepunguza hayo maddeni ili wenye deni waweze kulipa kabla ya yeye kupeana ofisi yake kwa mridhi wake. Alitenda hivyo. Aliyekuwa na deni la vipimo mia moja vya mafuta aliambiwa angeweza punguza deni lake hadi hamsini. Mwengine aliyedaiwa makanda mia ya ngano aliambiwa apunguze asilimia ishirini. Akaendelea hivo na orodha. Jinsi hiyo ya kutumia mamlaka yake ilimfanya awe rafiki miongoni mwa wale aliowapa kibali; bwana wake naye akamsifu na kumpongeza kwa hekima aliyo onyesha.

Kutumia huo mfano, Yesu kwa jinsi ile alikashifu mafarisayo kwa kuchukua mkondo tofauti. Alikuwa ametangaza kuwa waandishi na mafarisayo walikaa katika kiti cha Musa kama watafsiri wa sheria za Musa, na kwamba walikuwa wamefuata njia ya huyo wakili. Wangejifanya kuwa marafiki wa watu maskini na wenye dhambi kwa kujaribu kupunguza uovu wao, na kuwwahimiza wafanye wawezavyo kutimiza matakwa ya sheria. Badala yake waliweka mzigo kwa watu na kuwakatisha tamaa.

Haya yote kwa upande wao ilikua ni unafiki; kwa kuwa hawangesaidia maana walijua wao wenyewe hawangeweza kutimiza matakwa ya sheria, ambayo ni kipimo kamili cha uwezo, wa mtu mkamilifu. Nia yao nzuri ingefaa iwe kukiri uovu wao wenyewe, kujitahidi kutenda mema, kumsihi Mungu kuwarehemu na kufundisha watu pia kutenda hivyo. Kutenda hivo kungewafanya wawe tayari kupokelewa katika kibali cha injili mwishoni mwa dahari. Kama ilivyokuwa kawaida ya unafiki wao, walikuwa wakijizuilia kufanyika wanafunzi wa yesu na kutafuta neema na kusamehewa dhambi. Walikua pia wanawazuia wengine kuwa wafuasi kwa kudai kwamba ilikua inawezekana kupata kibali cha Mungu kupitia kulinda sheria.

**KUTUMIA MFANO HUU**

"Yesu akawaambia wanafunzi wake, Jifanyieni marafiki kwa mali ya udhalimu ili itakapokosekana – Mwisho wa uwakili wenu katika kifo- Matokeo ya wema wenu iwafanye mkubalike, katika ufufuo, kuingia katika makao ya milele". .—***Msitari wa 9***, nukuu.

Kuna nafasi ya mabishano kuelekea mafundisho ya mfano huu, lakini kwetu sisi inaonekana wazi kwamba yesu alimaanisha kwamba hekima ya wakili dhalimu inafaa kiugwa na wanafunzi wake katika kushiriki na mamoni, utajiri wa maisha ya sasa. Kuanzia wakati watu wa mungu wanajipeana kwa Mungu, wanapeana pia haki yao na nia yao ya ulimwengu huu, na kuwa tu mawakili wa muda wao, talanta, ushawishi, mali, n.k. "Nyinyi si wenu wenyewe; mmenunuliwa kwa gharama; kwa hivyo mtukuzeni Mungu." Jitahidi kutumia yote uliyonayo katika kumtumikia Mungu.

Hawa mawakili wa rehema za Mungu wana kibali chake kutumia vitu vyote vya dunia kuendeleza jitihada zao za kiroho; hawatahesabiwa dhalimu, kwa kuwa wanatumia fursa yao ya kidunia kujenga maisha yao ya kimbingu. Kwa upande mwingine hii itahesabiwa kwao kama uwakili wa haki; na kupatikana waaminifu katika kutumia vitu vya ulimwengu katika utumishi wa Mungu, hivyo wataweza kukabidhiwa mambo makuu ya usoni. Watapokelewa katika makao ya milele na wapewe ushiriki na Masihi katika Ufalme Wake mtukufu. Watakabidhiwa neema zote za Mungu watakazopewa wanadamu. Kujikana kwao katika wakati wa sasa, utayari wao wa kujitolea, itakuwa msingi wa idhini ya Kimungu na utukufu utakaofuata.

Ukosefu wa uaminifu katika wakati huu wa sasa kwa vitu vyenye thamani ndogo kunamaanisha kutokuwa waaminifu katika mambo makubwa yajayo.Yeyote atakayejipea vitu anazosimamia bila haki, hawezi aminika na mambo makuu ya usoni; na yeyote anayejitolea anaonyesha uaminifu wake na ukweli kwa Mungu, na kwake mambo makuu yatapeanwa. Je Mungu angeweza kuwakabidhi watu wasio waaminifu na wachoyo, na wenye tamaa mbaya, mambo ya utajiri wake wa usoni? Hakika La! Hawezi!

Yesu anauliza "ikiwa haujakuwa mwaminifu kwa mali ya mwingine, nani atakupa iliyo yako mwenyewe?"Kwa wafuasi wa Yesu, vitu vyote vya hizi nyakati za sasa ni vya Mungu"- vitu vya nyakati za sasa ni vya Mungu kwa sababu tumeviweka wakfu au kuvitoa kwake. Vitu vya maisha ya usoni ni vyetu. Kwa sababu Mungu ametuahidi hivyo. Lakini kuna masharti: kama uaminifu wetu na ukweli wetu. Ikiwa sisi sio waaminifu katika kushughulikia vitu tulivyoweka wakfu kwa Mungu, hawezi akatupea vile alivyosema kuwa vitakua vyetu kwa masharti. Kwa hivo ikiwa tutautumia vibaya na kuharibu uwakilishi wetu kwa kutumia hizo fursa kimakosa. Je tutatarajia Mungu apeane vitu alivyoahidi kwa walio waaminfu?

## KUTUMIKIA MABWANA WAWILI

Kuna nguvu mbili zinazovutana; moja ovu na ingine njema. Hizi zinajulikana kwa majina tofauti nazo ni kinyume katika kila njia. Mungu ndiye Bwana Mwema; Shetani ni bwana muovu; lakini kila mmoja ana wawakilishi na masilahi anuwai. Kwa hivyo Mungu, Roho Wake na mafundisho Yake, yanawakilishwa na neno upendo; ilhali shetani na njia zake huwakilishwa kwa uchoyo, tama mbaya na mamoni. Kupitia kuanguka kwa binadamu, ulimwengu wote umepoteza Roho wa Mungu na umekuwa chini ya utawala wa shetani kwa miaka mingi. Wote wamefanyika waovu au hata zaidi. Roho ya ubinafsi, tamaa, inayoongoza kwa udhalimu kwa ujumla, imeshika wanadamu, hivi kwamba hata baada ya kuona njia mbaya ni kwa shida sana ili nguvu yake juu yetu iweze kuvunjika. "Hatuwezi kufanya vitu ambavyo tungefanya."

Lakini haya ndio mapendekezo ya injili: Mungu ananatamani kuona nafsi aminifu ili kujiunga na Yesu katika kupeana baraka zake. Anazawadi thawabu hii kuu ya ufalme kwa wale watakao onesha kuwa wana Roho wa haki. Thawabu hii ni ya dhamana sana. Hakuna jambo litakaloweza kulingana nayo. Yeyote ambaye anakubali injili kwa hekima anaziacha dhambi na uovu na mambo yote ya matendo ya kimwili na yanayohusu shetani na anaweka uso wake kuelekea kwa Mungu, upendo na haki.

Lakini haitoshi kwamba ataingia katika agano kuacha ulimwengu na kuzifuata nyayo za Yesu. Haitoshi kwamba Mungu anakubali agano na kutoa Roho wake Takatifu. Kinahitajika ni zaidi ya hii. Lazima aonyeshe kuwa hapendelei tu mema kuliko maovu, lakini aonyeshe bayana kwamba kwa hiari anakubali kuteseka na kupoteza vitu vyote ili awe upande wa wema, upande wa Mungu.

Kisha huja majaribio na majaribu. Anatafuta kumtumikia Mungu na kupata thawabu ya utukufu, heshima na kutokufa katika ufalme na Yesu: lakini anapata mazoea kwa mwili wake kutafuta na kufurahia mambo ya mamoni na uovu. Hii huleta vita kubwa. Na mmoja au mwingine lazima ashinde. Kwa kuongezea katika kukua ndani ya neema, ufahamu na upendo, Kiumbe Kipya katika Kristo lazima ajijaze na himizo na ahadi za bibilia, la sivyo, atakata tama na aache kabisa kupinga ulimwengu, umwili na shetani.

Bwana ameahidi neema ya kutosha wakati wote wa hitaji, kwa waaminifu(**Waebrania 4:16**). Ana tuambia kwamba anajua sisi ni mavumbi. Anakumbuka umbo wetu (**Zaburi 103:14**), kwamba hatuwezi fanya ambayo tungependa kufanya. Lakini kwa wakati huo huo anatuhitaji tutende yote tuwezavyo, akituhakikishia kwa hayo yote neema yake itatutosha; hio ni kusema, kwa hayo yote uweza wake utatimilisha upungufu wetu huo (**2 Wakorintho 12:9**)

Katika mafunzo yetu, Yesu anatuonya mwanzo kwamba chaguo letu lafaa kua la milele; kwamba fikra kuwa twaweza mtumkia Mungu na mamoni kwa wakati mmoja ni makosa (**Mathayo 6:24**) **Luka 16:13**). Kwa jinsi vile tutakosa kuwa waaminifu kwa mmoja ndivyo hivyo tutakua waaminifu kwa wengine. Kwa hivyo ni juu yetu kuchagua kumtumikia Mungu tukihesabu ni tunuku kubwa sana kwetu na thawabu kubwa zaidi ya milele.

Hata hivyo, mengi yataegemea katika kipimo cha imani yetu. Tukiwa na imani katika Mungu, ahadi ya thawabu yake kuu na ahadi ya mwokozi kutupea neema yake na msaada wakati wa shida, itawezekana kwetu kupigana vita vizuri na kupata taji ambayo Bwana ametuwekea na wote wanaompenda kweli (**2Timotheo 4:7-8**).